

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

Supplement No. 7

20th February, 2026

SUBSIDIARY LEGISLATION

To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 7 Vol. 107 Dated 20th february 2026
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 70 la tarehe 20/2/2025

**SHERIA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA
MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI,
(SURA YA 268)**

MWONGOZO

**MWONGOZO WA UTENDAJI KAZI KWA MAWAKILI WA
SERIKALI NA MAAFISA SHERIA KATIKA KUTEKELEZA
MAJUKUMU YA UWAKILI WA MWAKA 2026**

MPANGILIO WA AYA

Aya Maelezo

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Fasili.
4. Malengo ya Mwongozo.
5. Masharti ya leseni ya uwakili.
6. Sifa za kuruhusiwa kutekeleza majukumu ya uwakili.
7. Utaratibu wa kuomba kibali.
8. Rejesta.
9. Hatua za kinidhamu.
10. Kufutwa kwa Mwongozo.

MAJEDWALI

Tangazo la Serikali Na. 70 (Linaendelea)

**SHERIA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA
MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI,
(SURA YA 268)**

MWONGOZO

(Umetengenezwa chini ya kifungu cha 27(4))

**MWONGOZO WA UTENDAJI KAZI KWA MAWAKILI WA
SERIKALI NA MAAFISA SHERIA KATIKA KUTEKELEZA
MAJUKUMU YA UWAKILI WA MWAKA 2026**

KWA KUWA Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na kifungu cha 8 cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye mwenye dhamana ya kuishauri Serikali katika masuala yote ya kisheria;

NA KWA KUWA kifungu cha 27 cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kinampa mamlaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa maelekezo au miongozo kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria katika Utumishi wa Umma kwa madhumuni ya kuhakikisha viwango na weledi katika kuhudumia wananchi na kuwa na mfanano wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kisheria;

NA KWA KUWA, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amepewa mamlaka kisheria, kuhakikisha kuwa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria katika Utumishi wa Umma, wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kutoa huduma kwa wananchi au kuhudumia umma kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanazingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali;

NA KWA KUWA, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameona ipo haja ya kuandaa mwongozo wa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria katika kutekeleza majukumu ya uwakili kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi katika maeneo mbalimbali ya kisheria yanayotekelezwa na mawakili ili kuboresha utoaji wa huduma kwa umma;

Tangazo la Serikali Na. 70 (Linaendelea)

HIVYO BASI, Mimi **HAMZA SAIDI JOHARI**, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ninatoa Mwongozo ufuatao:

- Jina 1. Mwongozo huu utajulikana kama Mwongozo wa Utendaji Kazi kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria katika Kutekeleza Majukumu ya Uwakili wa mwaka 2026.
- Matumizi 2. Mwongozo huu utatumika kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria waliopo katika Utumishi wa Umma.
- Fasili 3. Katika Mwongozo huu, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-
- Sura ya 21 “huduma za msaada wa kisheria” ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Msaada wa Kisheria;
- Sura ya 341 “leseni ya uwakili” maana yake ni leseni inayotolewa chini ya Sheria ya Mawakili, ambayo inatoa uhalali kwa mmiliki wake kufanya kazi za uwakili wa kujitegemea;
- Sura ya 268 “Afisa Sheria” ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- “mashauri binafsi” maana yake ni mashauri yasiyo na athari kwa Serikali yanayofunguliwa na, au dhidi ya, mtu binafsi au taasisi nafsi ambayo Serikali sio sehemu ya wadaawa, na yanajumuisha mashauri yanayohusu ndoa au talaka, mirathi na mashauri mengine yoyote yanayofanana na hayo;
- Sura ya 268 “Wakili wa Serikali” ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- “mgongano wa maslahi” maana yake ni hali ya Wakili wa Serikali au Afisa Sheria kuwa na maslahi binafsi ya kikazi ambayo yanaweza kuathiri, kuingilia au kuonekana kuathiri uwezo wake wa kutekeleza majukumu ya umma kwa ufanisi na uadilifu;
- Sura ya 21 “mtu asiye na uwezo” ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Msaada wa Kisheria;

Tangazo la Serikali Na. 70 (Linaendelea)

Sura ya 268 “Timu ya Serikali ya Sheria” maana yake ni Timu iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

“Utumishi wa Umma” inajumuisha utumishi katika Wizara, Tawala za mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Shirika la Umma au Shirika lingine lolote au taasisi ambayo Serikali ina maslahi.

Malengo ya
Mwongozo

4. Malengo ya kutolewa kwa Mwongozo huu ni-
- (a) kuongeza ufanisi wa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria katika maeneo mbalimbali ya kisheria wanayoyasimamia, ili kuboresha utoaji wa huduma kwa umma;
 - (b) kuwaruhusu Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria waliopo katika Utumishi wa Umma-
 - (i) kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa njia ya uwakilishi katika vyombo vya utoaji haki; na
 - (ii) kuendesha mashauri binafsi.

Masharti ya
leseni ya
uwakili
Sura ya 341

5.-(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 43 cha Sheria ya Mawakili, Wakili wa Serikali au Afisa Sheria hatapewa leseni ya uwakili kwa kipindi chote cha utumishi wake akiwa Wakili wa Serikali au Afisa Sheria.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1), Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza, iwapo kuna sababu maalumu, kutoa idhini kwa Wakili wa Serikali au Afisa Sheria kupewa leseni ya uwakili.

(3) Sababu maalumu kwa Wakili wa Serikali au Afisa Sheria kupewa idhini ya kuomba leseni ya uwakili zitajumuisha-

- (a) Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuridhika kwamba mwajiri wa Wakili wa Serikali au Afisa Sheria husika anahitaji huduma za uwakili;
- (b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuridhika kwamba hakuna mgongano wa maslahi;

- (c) Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuridhika kwamba utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa umma ni kwa mujibu wa Sheria ya Msaada wa Kisheria na miongozo itakayotolewa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya sheria; au
- (d) sababu nyingine yoyote ambayo Timu ya Serikali ya Sheria itaona inafaa.
- (4) Wakili wa Serikali au Afisa Sheria ambaye anahitaji kupewa leseni ya uwakili ataomba kibali kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia utaratibu ulioainishwa katika aya ya 7.
- (5) Maombi yaliyorejewa katika aya ndogo ya (4) yataeleza bayana sababu za Wakili wa Serikali au Afisa Sheria kuwasilisha maombi hayo.
- (6) Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya kupokea maombi yaliyowasilishwa chini ya aya ndogo ya (4) ataelekeza maombi husika kuwasilishwa katika Timu ya Serikali ya Sheria kwa ajili ya uchambuzi na mapendekezo.
- (7) Wakati wa uchambuzi wa maombi, Timu ya Serikali ya Sheria itazingatia masuala yafuatayo:
 - (a) athari za kibali kinachoombwa kwa majukumu ya mwombaji katika nafasi yake ya sasa;
 - (b) suala linaloombewa leseni ya uwakili kutokuwa na mgongano wa maslahi;
 - (c) idhini kutoka kwa mwajiri wa mwombaji inayoruhusu Wakili wa Serikali au Afisa Sheria kutekeleza majukumu ya uwakili; na
 - (d) suala lingine lolote ambalo Timu ya Serikali ya Sheria itaona linafaa kuzingatiwa.
- (8) Baada ya Timu ya Serikali ya Sheria kuchambua maombi itapendekeza kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali-
 - (a) kutoa kibali kwa mwombaji kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya uwakili; au
 - (b) kukataa maombi na kutoa sababu kwa mwombaji.
- (9) Baada ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupokea mapendekezo kutoka Timu ya Serikali ya Sheria,

Tangazo la Serikali Na. 70 (Linaendelea)

atamjulisha mwombaji kuhusu uamuzi wake ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kufanya uamuzi.

(10) Kibali kinachotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kitatumika ndani ya muda wa miaka mitatu na mwombaji anaweza kuomba tena.

(11) Bila kuathiri aya ndogo ya (10), Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kusitisha wakati wowote kibali kilichotolewa iwapo mwombaji atakiuka masharti ya Mwongozo huu.

Sifa za
kuruhusiwa
kutekeleza
majukumu ya
uwakili

6. Wakili wa Serikali au Afisa Sheria anaweza kuruhusiwa kutekeleza majukumu ya uwakili iwapo-

- (a) amekidhi sifa za kufanya shughuli za uwakili kama zinavyoelekezwa katika sheria nyingine za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (b) ameajiriwa na kuthibitishwa kazini katika Utumishi wa Umma kwa masharti ya ajira ya kudumu;
- (c) amesajiliwa na kuorodheshwa katika mfumo wa Usimamizi wa Taarifa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- (d) amelipia ada ya uanachama wa Chama cha Mwakili wa Serikali kwa kipindi cha angalau miaka miwili mfululizo; na
- (e) hana mgongano wa maslahi na mwajiri wake katika utekelezaji wa majukumu ya uwakili.

Utaratibu wa
kuomba kibali

7.-(1) Wakili wa Serikali au Afisa Sheria mwenye sifa zilizoainishwa katika aya ya 6 atapaswa kujaza fomu ya maombi iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Mwongozo huu na kuwasilisha katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia mfumo wa Usimamizi wa Taarifa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (OAGMIS).

(2) Fomu ya maombi itaambatishwa na-

- (a) nakala ya barua ya ajira;
- (b) nakala ya barua ya kuthibitishwa kazini; na
- (c) tamko la kutokuwa na mgongano wa maslahi kama lilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Mwongozo huu.

*Mwongozo wa Utendaji Kazi kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria
Katika Kutekeleza Majukumu ya Uwakili*

Tangazo la Serikali Na. 70 (Linaendelea)

Rejesta

8.-(1) Kutakuwa na Rejesta ambayo taarifa za Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria wanaoruhusiwa kutekeleza majukumu ya uwakili katika Utumishi wa Umma zitaingizwa na kuhifadhiwa.

(2) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali atahifadhi na kutunza Rejesta ya Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali wanaoruhusiwa kutekeleza majukumu ya uwakili katika Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Mwongozo huu.

Hatua za
kinidhamu

9. Wakili wa Serikali au Afisa Sheria anayekiuka masharti ya Mwongozo huu anatenda kosa la kitaaluma na hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake kama ilivyoanishwa katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Sura ya 268

Kufutwa kwa
Mwongozo
TS. Na
1008 la 2020

10. Mwongozo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Utekelezaji wa Majukumu kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria Wanaofanya Kazi za Uwakili, unafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya aya ya 7(1))

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI NA LESENI YA KUTEKELEZA MAJUKUMU YA UWAKILI

SEHEMU A: MAELEZO YA MWOMBAJI

Jina Kamili
Cheo/Wadhifa:
Namba ya Ajira (Check No.)
Wizara/Taasisi/Shirika/Wakala/Idara:.....
Mahali pa Kazi (Anuani Kamili):
Namba ya Simu: Barua Pepe:
Namba ya Uwakili wa Serikali katika Orodha ya Mawakili wa Serikali:.....

*Mwongozo wa Utendaji Kazi kwa Mwakili wa Serikali na Maafisa Sheria
Katika Kutekeleza Majukumu ya Uwakili*

Tangazo la Serikali Na. 70 (Linaendelea)

Namba ya Uwakili katika Orodha ya mawakili (TLS Roll No)

.....

Saini ya

Mwombaji:

Tarehe:

TAARIFA ZA MWAJIRI

Jina la Mwakiri:

Anuani ya Mwakiri:

S.L.P:

Barua pepe:

Wilaya:

Mkoa:

SEHEMU B: TAJA SABABU YA MAOMBI

.....

.....

.....

SEHEMU C: TAMKO LA MWOMBAJI

Mimi natamka kuwa maelezo yote

niliyotoa ni sahihi na kweli.

Saini ya Mwombaji:

Tarehe: Mwezi: 20.....

SEHEMU D: RIDHAA YA MWAJIRI

Jina:

Cheo:

Nimeridhia/Sijaridhia

Saini.....

MUHURI WA MWAJIRI

KWA MATUMIZI YA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Maoni ya Timu ya Serikali ya Sheria:

.....

.....

.....

.....

.....

Mapendekezo ya Timu ya Serikali ya Sheria:

.....

*Mwongozo wa Utendaji Kazi kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria
Katika Kutekeleza Majukumu ya Uwakili*

Tangazo la Serikali Na. 70 (Linaendelea)

RIDHAA YA MWANASHERIA MKUU
KURUHUSIWA/KUTORUHUSIWA

Kwa kuzingatia aya ya ya Mwongozo wa Utendaji Kazi kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria Katika Kutekeleza Majukumu ya Uwakili, nimetoa ridhaa/sijatoa ridhaa kwa maombi ya kupatiwa leseni ya uwakili.

Sababu za kukataliwa kwa maombi ni hizi:

.....
.....
.....

Tarehe..... Mwezi.....20.....

.....
MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI



*Mwongozo wa Utendaji Kazi kwa Mwakili wa Serikali na Maafisa Sheria
Katika Kutekeleza Majukumu ya Uwakili*

Tangazo la Serikali Na. 70 (Linaendelea)

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya aya 7(2)(c))

TAMKO LA KUTOKUWA NA MGONGANO WA MASLAHI

Mimi..... natamka kwa dhati na kwa uaminifu
kama ifuatavyo: (hapa bainisha mambo yanayotamkwa)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Mimi..... ninatoa tamko hili kwa dhamira
njema nikiamini kuwa ni kweli na kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Viapo na Matamko
ya Kisheria, Sura ya 34.

Tamko hili limetolewa na kusainiwa na
ambaye ninamfahamu binafsi/ ametambulishwa
kwangu na

ambaye namfahamu)

Tamko

tarehe mwezi..... mwaka 20....

Mtoa

.....
(Saini ya mpokea tamko)

Dodoma,
12 Februari, 2026

HAMZA SAIDI JOHARI
Mwanasheria Mkuu wa Serikali